

# Mshukuruni Bwana

Zb.106, 23-31

Musique & Harmonisation: Gervais CIZA

$\text{♩} = 80$

S  
A

Mshuku-ru-ni Bwa - na kwa-ni ye-ye pe - ke a - me - te - nda ma - ja - bu.

T  
B

8

1. Wamshukuru Bwana sababu ya **wema** wake,  
na kueleza matendo yake kwa shangwe,  
hao waliona matendo ya Bwana,  
na maajabu yake **vilindini**.
2. Aliamuru akavumisha upepo **wa** zoruba,  
nao ukarusha juu mawimbi **ya** bahari,  
wakapanda juu angani wakashuka chini **vilindini**,  
maarifa yote yake **kafutika**.
3. Wakamlilia Bwana katika mahangaiko yao,  
akawatoa katika masumbufu yao,  
akaituliza zoruba iwe upepo mwanana,  
mawimbi ya bahari yake **kanyamaza**.
4. Wakafurahi kwa kuwa yametulia,  
akawapeleka katika bandari waliyotamani,  
wamshukuru Bwana kwa **wema** wake,  
na maajabu yake kwa ajili ya **wanadamu**.

Usage 12<sup>e</sup> dim.ord.B